# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE**

Email: sekondarimajimoto@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI MAJIMOTO,
S. L. P 158,
**MPANDA- KATAVI.**

Office No: 0745761077

Mob: 0766242319

*Kwa kujibu tafadhali rejea:*
*Kumb. Na.* MMSS/ADM/F1/2022/__________

---

Mwanafunzi________________________________________

YAH: **MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021.**

1. Nafurahi kukuarifu rasmi kuwa umechaguliwa kuingia Kidato cha kwanza (1) katika Shule hii.
2. Shule ipo ndani ya Halmashauri ya Mpimbwe kata ya Majimoto kilomita 26 kutoka Ofisi za Halmashaurina kilomita 1.5 toka kituo cha mabasi Majimoto. Hii ni Shule ya Kutwa kwa wavulana na wasichana
3. Shule itafunguliwa Jumatatu ya tarehe **- saa 1:00 asubuhi**.Kama hutofika hadi tarehe **-/01/2020** nafasi yakoitachukuliwa namwanafunzi mwingine.

**SHERIA ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Sheria hizo ni kama ifuatavyo:

1. Heshima na adabu kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla.
2. Utii kwa Walimu, Wafanyakazi wasio Walimu na Viranja.
3. Kuwahi kufika Shuleni na kutoondoka Shuleni kabla ya kutawanyika au Shule kufungwa.
4. Kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku za Shule.
5. Kuwahi katika kila wito (utii kwa kengele).
6. Kuvaa sare ya Shule madarasani, muda wa kazi na michezo.
7. Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
8. Hairuhusiwi kutembelea vilabu vya pombe,majumba ya starehe wala nyumba ya wageni.
9. Ulevi wa aina yeyote ni marufuku.
10. Ugomvi na matusi ni mwiko.
11. Wizi, kuharibu mali/ kifaa cha Shule au kuandika maandishi na michoro kwenye kuta za shule, milango n.k ni marufuku.
12. Kila mwanafunzi anatakiwa awe msafi.
13. Ni mwiko kutupa taka/ karatasi au uchafu ovyo.
14. Urafiki wa kimapenzi hauruhusiwi Shuleni.
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda nyumbani kwa Wafanyakazi bila ruhusa.
17. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vyombo vya umeme hosteli/ darasani au mahali popote ndani ya Shule.
18. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na **Simu ya mkononi**au “**simcard”**Shuleni, Adhabu kali itatolewa ikiwemo kulipia uharibifu wa Mfumo wa Umeme na Mzazi kumhamisha Mwanafunzi husika.
19. Ni marufuku kuvaa kofia, heleni, mkufu, kanga, pete, sketi fupi au za kubana/ mipasuo au kuvaa suruali za kubana na mtepesho.
20. Marufuku kufuga nywele ndefu, kupaka rangi kucha au nywele, kujichubua

21. Mwanafunzi kutofanya jaribio au zoezi au kutofanya kazi aliyopewa au kutoandika nukuu (notisi) a;izopewa na mwalimu wa somo ni KOSA KUBWA SANA, ambalo halina msamaha.
22. Mwanafunzi haruhusiwi kuficha taariifa za uovu wowote ule aliouona au kuusikia.
23. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi kitabuni, katika dawati, meza, viti, au kwenye kuta za majengo ya shule.
24. Ni kosa kwa mwanafunzi kumkimbia mwalimu au mfanyakazi yeyote wa shule.
25. Ni kosa kwa mwanafunzi kutosalimia walimu, wafanyakazi wa shule au watu wakubwa pamoja na kutopokea mizigo.
26. Wastani wa shule ni 50% atakayepata chini ya wastani huu atapata adhabu kali bila msamaha.
27. Kila mwanafunzi ashiriki kwenye vikundi vya dini kama vile; TYCS,ASA,CASFETA,UKWATA na TAMSYA na kuheshimu kikundi cha dini anachosali mwenzake.

**MIIKO MAALUMU: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

(a). Kashfa ya aina yoyote kwa Taifa kama kudharau mambo ya Kitaifa (sikukuu zaKitaifa, mikutano, wimbo wa Taifa, bendera ya taifa, maandamano, nk.
(b). Wizi (kuiba).
(c). Kuoa au Kuolewa.
(d). Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(e). Kutohudhuria Shule kwa muda mrefu (utoro) bila taarifa.
(f). Kupigana au Kupiga.
(g). Kuchochea ghasia/ kugoma au kuongoza migomo na kuvunja amani na usalama washule au watu.
(h). Kuvuta sigara, bangi au dawa za kulevya na kunywa pombe,
(i). Kuendesha magendo au ulanguzi wa aina yoyote.
(j). Kosa la jinai, kosa likithibitishwa na polisi, au mahakamani.
(k). Kulala nje ya shule bila ruhusa wakati wa kambi kwa madarasa ya Mitihani.
(l). Kugomea adhabu.
(m). Kuwa na simu ya mkononi Shuleni.
(n). Ubakaji, ulawiti, ushoga na usagaji.
(o). Kumpa mimba msichana ndani au nje ya shule.
(p). Kumiliki simu au laini ya simu ukiwa shuleni.

**SARE YA SHULE:**

i. **(a) Wavulana**; Suruali mbili [2] rangi **kijani kibichi** zenye mifuko miwili ya pembeni kwa mbele, mfuko mmoja nyuma upande wa kulia, Suruali iwe saizi ya kawaida isiyoshika mwili (modo haitakiwi),**inchi 18** upana chini,urefu usawa wa kuanzia soli ya kiatu, isiwe na urembo wowote. (mlegezo hautakiwi).
**(b) Wasichana;** sketi mbili kijani kibichi, zenye urefu wa sentimita 26 kutoka kwenye goti au Zaidi, iwe ya linda box, linda 8, linda moja kubwa mbele na nyuma na matatu upande wa kulia na matatu upande wa kushoto. (IWE NDEFU SANA, SKETI FUPI HAZITAKIWI)
ii. Tai moja ya **kijani kibichi** ndefu usawa wa tumbo isiyo na mchanganyiko wa rangi nyingine yoyote.
iii. T-shirt moja maalumu ya kijani kibichi yenye nembo ya shule. Zinapatikana shuleni kila moja shilingi 12,000/=
iv. Mashati mawili meupe (tetroni) ya mikono mifupi mfuko mmoja kushoto.
v. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba jozi mbili, visiwe na visigino virefu. “Safari boots na viatu vya wazi” haviruhusiwi kabisa.
vi. Soksi (stockings) jozi mbili au zaidi za rangi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
vii. Mkanda wa ngozi mweusi wenye upana wa kawaida (usiwe na chater yoyote) kwa wavulana.

viii. Sweta moja la rangi ya kijani kibichi lenye kola ya “V”. Linapatikana shuleni.

ix. Nguo za michezo za mwanafunzi aje na:-

a) Tracksuit ya rangi ya kijivu. (c) Bukta ya rangi nyeusi

b) T-Shirt ya rangi ya Kijivu. (d) Raba kwa ajili ya michezo

**USAFI BINAFSI WA MWILI:**

- Kufua nguo zako za Shule kila wakati ni lazima.
- Nywele fupi za kuchana kwa kitana kidogo.
- Ndevu na mustachi havitakiwi kabisa.
- Kuoga kila siku ni lazima
- Huruhusiwi kufuga kucha wala kupaka rangi kucha.
- Kuvaa kofia, bangili, hereni, kipini, kidani, (mkufu) na kikuku haviruhusiwi shuleni.

**AJE NA VIFAA VIFUATAVYO:**

i. **Vifaa vya Usafi:**Ufagio wa ndani (Hard broom moja au Soft broom moja, Jembe na mpini wake moja, Fagio la Chelewa lenye mpini moja, Ndoo moja ndogo ya plastiki iliyo safi.

ii. **Vifaa vya Darasani:** Madaftari tisa (9) (Counter book three (3) quires au four (4) quires), kalamu ya bluu/ nyeusi, Mathematical set na Begi la Darasani [School bag].

iii. **Ream moja (A4)** Kwa ajili ya majaribio na mitihani mbalimbali.

**HITIMISHO:**

i. Unapaswa kuja na fomu zilizoambatanishwa na barua hii zikiwa zimejazwa vizuri. Fomu hizo niviambatanisho ‘A’ na ‘B’.

ii. Shule hii ni ya Kilimo, Jiandae kujifunza kulima na kufuga kwa vitendo.

iii. Kufanya **majaribio**, **mitihani** na kuhudhuria maandalizi ya jioni [Evening preparation for NECTA classes] ni **LAZIMA** sio hiari.

Nakutakia heri na mafanikio ukiwa katika Shule hii.

***Ni matumaini yangu daima utatii <u>sheria</u>, <u>taratibu</u>na<u>kanuni</u> za Shule ili uje uvune kile kilichokuleta hapa, ambacho ni <u>ELIMU.</u>***

HONGERA NA KARIBU SANA

.................................

MASHAURI L. H

MKUU WA SHULE

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALIMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE**
**SHULE YA SEKONDARI MAJIMOTO**

**FOMU YA UTHIBITISHO NA MKATABA WA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAJIMOTO.**

*Makubaliano ya mkataba kati ya Mzazi,mwanafunzi na shule yatatekelezwa kama yalivyo kwa lengo la kufuta daraja sifuri na nne[ division 0 and iv]*

***Picha ya Mwanafunzi***

**[A]. IJAZWE NA MWANAFUNZI:**

1. Jina kamili la Mwanafunzi ………………………………………………………..
2. Uraia ……………… 3. Kabila ……………..…. 4.Dini: …………………...
5. Tarehe ya kuzaliwa ……….…………… Wilaya:…………..……… Mkoa: …….……………..
6. Shule uliyohitimu darasa la saba………………………... Namba ya mtihani …………………….
7. Umbali wa kutoka nyumbani hadi Majimoto sekondari ni kilomita ………………………………….

Mimi ………………………………………………nikiwa na akili timamu na maarifa, nakubali kupokea nafasi niliyopewa ya kidato cha …………… Naahidi kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Masharti mengine yote ya Shule,Ikiwemo kutopata alama **F** na **0** darasani, kutomiliki simu ya mkononi shuleni, utoro wa vipindi na kudharau baadhi ya masomo, majaribio na mitihani..Endapo nitaingia kwenye makosa hayo mabaya naomba mzazi/mlezi wangu anitafutie shule nyingine nakunihamisha mara moja. Nakubaliana na hoja zilizoanishwa hapo juu na kwenye fomu ya kujiunga na shule ya Sekondari **Majimoto**.

Jina la mwanafunzi…………………..………………… Sahihi ya Mwanafunzi………………………

Tarehe ya mkataba ………………………………….

**[B]. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/ MLEZI ATAKAYETAMBULIWA NA SHULE.**

***Picha ya Mzazi/ Mlezi***

1. Jina kamili la Mzazi/ Mlezi ……………………………………………………
2. Anuani kamili ya Mzazi/ Mlezi ……………………………………….………..
3. Kazi unayofanya Mzazi/ Mlezi ……………………………………………………
4. Namba ya simu: [a]Nyumbani…………………[b]. Mkononi …………….…….

[c] Tarafa ……………….. [d] Wilaya …………………… [e]. Mkoa………………..

Mimi ……………………………….………Mzazi/ Mlezi wa …………………….…………….…

Nikiwa na akili timamu, nimesoma vyema Sheria, Taratibu na Kanuni za Shule, Nakubali/Sikubali, mwanangu ajiunge na Shule ya Sekondari Galanos. Endapo Mwanangu ataenenda kinyume na Sheria/ taratibu za Shule na kupatikana na kosa la kupata alama **F** na **0**, kumiliki simuya mkononi shuleni, na kushiriki utoro wa vipindi, kukwepa mitihani na kudharau baadhi yamasomo, kama ilivyoainishwa hapo juu nakubali nikabidhiwe kijana wangu ili **nimtafutie** shulenyingine ili kuepusha madhara na majanga kwa wanafunzi wengine na niweze kumsimamia kwakaribu na sitakuwa na pingamizi ya aina yoyote juu ya jambo hili kwani nafahamu fika kwambakilichomleta shule ni kusoma na si vinginevyo.

Pia kwa mujibu wa **waraka wa ELIMU Namba3 wa mwaka 2016** kuhusu utekelezaji wa elimu msingi bila malipo kipengele namba 3.10 (i – iv) kinachozungumzia wajibu wa mzazi, nipo tayari kuchangia chakula cha mwanafunzi kama ifuatavyo:-

Mahindi debe mbili (2), sukari kilo mbili (2), maharage kilo kumi na tano (15), mchele kilo ishirini (20) na fedha taslimu shilingi elfu thelathini (30,000/=) kila muhula. Endapo sitachangia chakula nipo tayari kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi …………………………….………. Tarehe ….….………………….…

**C. UTHIBITISHO WA SERIKALI ZA KIJIJI**

Jina la Mwenyekiti wa Kijiji au Afisa Mtendaji wa Kijiji……………….…………………………...…. Sahihi………………………Namba ya Simu…….………………………..Muhuri…………………...

*KIAMBATANISHO "B"*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

## *STUDENT MEDICAL CERTIFICATE*

(To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster of Majimoto Secondary School P. O. Box 158, MPANDA-KATAVI)

To the Medical Officer,

………………………………………….

………………………………………….

………………………………………….

RE: ______________________________________________________________________

Please, examine the Student mentioned above and comment in his health by responding to the following items. Kindly put a Tick (v) or Cross (x) in front of either YES or NO as you find appropriate.

........................
HEADMASTER

Does a student have problems in connection with?

a) Sight? (1) No (2) Yes

If yes, state ……………………………………………………………………………

b) Hearing? (1) No (2) Yes

If yes, state ……………………………………………………………………………

c) Speech? (1) No (2) Yes

If yes, state ……………………………………………………………………………

d) T. B (1) No (2) Yes

If yes, state ……………………………………………………………………………

e) Blood pressure? (1) No (2) Yes

If yes, state ……………………………………………………………………………

f) Any Physical disability? (1) No (2) Yes

If yes, state ……………………………………………………………………………

Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this School?

(1) No (2) Yes. If no, please state reasons.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

*Date ……………………………... Name and Signature of M. O ………………………………………..*

*Designation and stamp …………………………………………………….*